# Serikali yawekeza bilioni 60/- kuwainua wavuvi

Na MWANDISHI WETU

SERIKALI imewekeza sh. bilioni 60 katika sekta ya uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, lengo likiwa kuinua kipato cha wananchi.

Kauli hiyo, ilitolewa jijini Mwanza mwishoni mwa wiki kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayesimamia Sekta ya Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, wakati wa ujio wa mabalozi wanane kutoka Umoja wa nchi za Ulaya (EU) katika Kampasi ya Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi Tanzania (FETA).

Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani, Profesa Mohammed Sheikh aliyemuwakilisha kwa niaba ya katibu mkuu, alisema fedha hizo zimewekezwa kuongeza uzalishaji wa kuinua boti na wavuvi wafugaji wafike eneo la maji ya kina kirefu kuvua samaki, wapate kipato.

Profesa Sheikh alisema ujio wa mabalozi hao ni ule wa kawaida kujionea namna utekelezaji wa miradi hiyo ambayo wanashirikiana na serikali kuwaondoa wavuvi katika matumizi ya zana za zamani za uvuvi na kutumia njia ya vizimba kwa kufuga samaki wengi wapate vipato zaidi.

## MTENDAJI MKUU FETA

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa FETA, Dk. Semvua Mzighani alisema ufugaji samaki kwa njia ya vizimba unakuwa kwa kasi na serikali imewekeza fedha hizo kuwawezesha vijana kuchangamkia fursa kupitia Ziwa Victoria.

Dk. Mzighani alisema wanatoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, wanashauri wanaohitaji kujifunza namna ya kufuga samaki kwa njia ya vizimba wajiunge kujifunza jinsi ya kutengeneza vizimba, namna ya kuviweka ziwani, kupata mbegu bora za samaki, kuzikuza na kuzihifadhi wasiharibike baada ya kuvuliwa.

Alisema kumekuwa na mwitikio mkubwa wa watu kujifunza namna ya kufuga samaki kupitia vizimba tayari wapo ambao wameanza kuwekeza katika Ziwa Victoria.

Aliwaomba watu wengi zaidi wajitokeze hasa vijana kuchangamkia fursa hiyo.

Naye, mmoja wa wafugaji samaki kwa njia ya vizimba katika Ziwa Victoria ambaye amepata elimu FETA, Mpanju Elpidius, aliwaasa vijana wenzake kuchangamkia fursa hiyo kwa kuanza na kidogo walichonacho wafikie malengo yao.

Alipongeza serikali kupitia wizara hiyo kutenga fedha za kuwakopesha vijana kwa masharti nafuu kufuga samaki kwa njia ya vizimba na kuziomba benki zilizopo nchini kuiga mfano wa serikali kwa kuwaamini vijana na kuwakopesha kwa masharti nafuu.

Baadhi ya mabalozi kutoka nchi za Ulaya waliotembelea miradi inayotekelezwa na FETA ukiwemo wa utoaji elimu ya ufugaji samaki kwa njia ya vizimba katika ziwa hilo, wameridhishwa na namna fedha walizowekeza zinavyotumika kuhamasisha vijana kujitokeza kwa wingi na kuomba serikali kuwasimamia waturnie kwa malengo yanayotarajiwa.

Umoja wa Nchi za Ulaya, umewekeza FETA sh. milioni 800 kwa kukuza sekta ya uvuvi kupitia ufugaji samaki na uwekezaji umefanyika katika mwambao mitaala.




Mtambo wa

# Ukame waleta hasara kwa wafugaji

Mussa Juma, Mwananchi
mjuma@mwananchi.co.tz

**Monduli.** Wafugaji wilayani Monduliwamepata hasara ya Sh18.3 bilioni baada ya mifugo yao 127,786 kufa kwa kukosa malisho kutokana na ukame uliojitokeza mwaka 2021/22 huku Serikali ikipoteza Sh487.3 milioni zitokana zo na kodi na tozo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Monduli, Isack Copriano alitoa taarifa hiyo jana alipozindua mradi wa nyanda ya malisho unaotekelezwa na shirika la Utafiti na Maendeleo (Cords) ukifadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Copriano alisema mabadiliko ya tabianchi ndio chanzo cha vifo vya mifugo hiyo hivyo mradi huo umekuja wakati muafaka.

"Tunashukuru sana kwa mradi huu kwani utakuwa na manufaa makubwa kwa wafugaji wa Monduli ambao wameathirika sana na mabadiliko ya tabianchi na taarifa zinaeleza mwaka huu hali itakuwa mbaya zaidi," alisema.

**Sh18.3 bil**

**Hasara waliyopata wafugaji wilayani Monduli kutokana na kufa kwa mifugo yao.**

**300,000**

**Thamani iliyokadiriwa ya kila ng'ombe aliyekufa kutokana na kukosa malisho msimu huu.**

Kaimu Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Monduli, Yandu Marmo alisema kati ya mifugo hiyo 127,786 kulikuwa na ng'ombe 41,964 na mbuzi 31,213 pamoja na kondoo 54,609.

"Hii hasara tulipiga kwa makisio ya chini mfano tuliweka kama ng'ombe wangekuwa hai wangeuzwa kwa Sh300,000 kila mmoja hivyo hasara ni kubwa kwa wafugaji," alisema.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mkurugenzi wa Cords, Lilian Looloitai alisema wanatarajia mradi huo utawanufaisha zaidi ya waafugaji 1,476.

"Mradi huu tutautekeleza katika vijiji vitatu ambavyo ni Emairele, Emurua na Eluai hapa Monduli," alisema.

Akiuelezea mradi huo, Profesa Ismail Selemani alisema kabla ya kupanda nyasi katika maeneo hayo utafiti umefanyika na kuzibaini aina zistahimilizo ukame na kustawi vizuri katika udongo huo.

Profesa Selemani alisema lengo la mradi huo ni kuboresha maisha ya wafugaji na, kuendelea na kusimamia malisho.

Mkurugenzi wa Shirika Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF), Zakaria Faustine linaloratibu mradi huo aliwataka wafugaji kujifunza njia bora za kuandaa malisho.

"Haya majani ambayo yatapandwa katika nyanda za malisho yanapatikana maeneo mbalimbali na ukipanda mara ya kwanza hautalazimika kupanda kila mwaka kama mazao mengine," alisema Faustine

10:36
You
Just now




# Tukabiliane na mabadiliko ya tabianchi kunusuru mifugo

Mabadiliko ya tabianchi mbali ya kuleta athari nyingi katika shughuli za watu duniani, huathiri baadhi ya sekta ikiwamo ya mifugo.

Kwa mfano, mara nyingi mifugo imekuwa ikifa kwa kukosa malisho wakati wa ukame na hivyo kuwaacha wafugaji wakiwa na hasara kwa kupoteza idadi kubwa ya mifugo.

Mwaka jana zaidi ya mifugo 60,000 iliripotiwa kufa kwa njaa hapa nchini, na sababu kubwa ilitokana na ukame uliokumba baadhi ya maeneo nchini.

Mbali ya mifugo kufa, mabadiliko ya tabianchi yamesababisha wafugaji kukosa fedha za kutosha, kwani wanalazimika kuuza mifugo yao kwa bei ya kutupa ili kuepukana tu na kadhia ya kuwaacha wafe kwa kukosa maji na malisho.

Hapa ndipo umuhimu wa Serikali kuwekeza zaidi katika kuwezesha wafugaji wanapata malisho wakati wote, unapohitajika katika kuwaokoa wafugaji kuingia katika umasikini.

Kwa kufanya hivyo, hata migogoro ya ardhi itapungua kwa sababu wafugaji hawatakwenda kuchunga tena katika mashamba ya wakulima na hata kupeleka mifugo yao kwenye hifadhi.

Leo hii tunashuhudia namna uzalishaji wa maziwa kutoka kwenye ng'ombe na mbuzi unavyoshuka, kutokana na mifugo hiyo kukosa lishe inayostahili baada ya malisho kupungua ama kukosekana.

Bajeti ya mwaka 2022/2023, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliidhinishia Sh268.25 bilioni, huku zaidi ya robo tatu ya bajeti hiyo ambayo ni Sh209 bilioni ikielekezwa katika miradi ya maendeleo.

Bajeti hiyo ilikuwa ni ongezeko la Sh100.25 bilioni ya bajeti ya mwaka 2021/2022, ambapo wizara hiyo iliidhinishiwa Sh168 bilioni.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki wakati akiwasilisha bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023, alisema watajenga miundombinu ya uboreshaji wa malisho na maji, sambamba na kuanzisha madarasa darasa ya kilimo cha nyasi 100. Haya yatatumika kama sehemu ya kujifunzia kwa wafugaji.

"Tunalenga badala ya wafugaji kuhamama waweze kuwa na mahali pamoja kwa kuwa na uhakika wa kupata malisho pale pale pia wakiwa na uhakika kupata maji," alisema.

Licha ya jitihada hizo, kuna umuhimu bado kwa Serikali kuongeza jitihada ya kuwekeza zaidi katika eneo la malisho, ili kuwasaidia wafugaji kuondokana na changamoto ya mifugo kufa.

Mkakati usiwe kuongeza bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, bali kuongeza bajeti ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hasa kwa kuongeza uzalishaji wa malisho.

Tukishaongeza bajeti, fedha hizo zitumike katika kuibua mashamba ya nyasi ambayo yatawezesha wafugaji kuwa na uhakika wa malisho kwa kipindi chote cha mwaka, hatua itakayowafanya waepukane na vifo vya mifugo ambavyo vimekuwa vikisikika kila mara wakati wa ukame.

Ili kuwezesha hayo, ni muhimu kwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (Taliri), ambayo imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali za malisho ikaongezewa fungu la bajeti kwa ajili ya kujikita kwenye eneo hilo, ili kuwezesha uzalishaji wa nyasi zitakazoongeza uzalishaji kwenye bidhaa zinazotokana na ng'ombe na mbuzi.

Hili litatusaidia pia kuongeza kiasi cha fedha za sekta hii zitakazokwenda kuchangia katika pato la Taifa.

> **Licha ya jitihada hizo, kuna umuhimu bado kwa Serikali kuongeza jitihada ya kuwekeza zaidi katika eneo la malisho, ili kuwasaidia wafugaji**

Mkurugenzi Mkuu wa Taliri, Profesa Erick Komba amesema mwaka jana walisambaza tani 18,000 na mwaka huu wamesambaza mikate ya nyasi tani 20,000, lakini mahitaji ni tani 500,000 ili kuokoa mifugo isife kutokana na ukame.

Pamoja na jitihada hizo za Taliri, mahitaji bado ni makubwa katika eneo hilo la malisho na jitihada zielekezwe pia kuwawezesha wafugaji kulima wenyewe malisho na kuhifadhi kwa teknolojia bora.

Wakiwezeshwa kwenye hilo, kutasaidia waondokane na tabia ya kuhamahama na kuepusha migogoro ya mara kwa mara na wakulima.

Bado hatujachelewa kwa sababu uandaaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 unaendelea kufanyika, hivyo ni wakati mzuri wa Serikali kuangalia eneo hili ambalo litatuwezesha kuongeza kiasi cha fedha kinachochangiwa katika pato la Taifa kutokana na sekta hii.

Wabunge nao wanapaswa kuangalia sekta hii inapokuja bungeni, ili bajeti yake iweze kuwawezesha hawa wafugaji kuondokana na changamoto ya malisho.

Wabunge wanategemewa kwa kiasi kikubwa, kwa sababu wao ndio wapitishaji wa bajeti na wanaweza kuishauri Serikali kwa namna wanayoona inafaa.

*Sharon Sauwa ni mwandishi wa Mwananchi mkoani Dodoma 0746-999966.*

CamScanner